
Dr. Wilfred D. Kiboro *Mwenyekiti*

# Taarifa ya Mwenyekiti

**Wapendwa Washikadau,**

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, nina furaha kubwa ya kuwawasilishia utendakazi wa kifedha wa Shirika la mwaka uliomalizikia tarehe 31 Desemba, 2020.

Mwaka wa 2020 ambao hautasahaulika, usio kifani na usioweza kulinganishwa. Ulimwengu uliathiriwa na tandavu ambalo kizazi cha sasa hakijawahi kupitia. Tandavu hili limepindua dunia juu chini, na kulazimisha mataifa kadhaa kufunga baadhi ya shughuli au kufunga shughuli zote kabisa. Usafiri wa ndege, za humu nchini na zile za kimataifa, ama ulisimamishwa au ulifanywa kuwa vigumu zaidi, na baadhi ya viwanda vilifungwa huku vingine huenda vikaanguka.

Hatua hizi zimevuruga maisha yetu kwa njia ambayo yeyote miongoni mwetu hajawahi kupitia awali, kuzuia biashara na mifumo ya usambazaji wa bidhaa, na kusababisha watu wengi kupoteza kazi au kupunguziwa mishahara, kufanya kazi nyumbani, au kuenda likizo bila malipo, huku biashara zikijaribu kumudu janga hili la kipekee. Hata hivyo, kuvurugwa kwa shughuli kulikuwa na matokeo mengine chanya; hali hii ililazimisha biashara kuweka mikakati mipya kwa kuongeza kasi ya mageuzi ya kidijitali.

Tunasherehekea na kukaribisha maendeleo ya kutolewa kwa chanjo za Covid-19 kwa zamu huku pia tukitambua aina mpya za tandavu ambazo zimekuwa hatari kwa juhudi za sasa ili kukabiliana na tishio hili la maisha. Hivyo, katika kipindi hiki, usalama na ustawi wa wafanyakazi, familia, washirika, wateja wetu na washikadau wengine katika masoko yetu yote unaendelea kuwa kipaumbele bora kwetu kwa kufuata miongozo iliyotolewa na Serikali. Shirika lina Kikosi cha Usimamizi Endelevu wa Kibiashara cha kushughulikia masuala yoyote yanayotokana na tandavu hili. Tutaendelea kutoa msaada wetu imara kwa washikadau na Serikali katika Afrika Mashariki.

## Mazingira ya Kiuchumi

Nchi za Afrika Mashariki zote zilipitia aina fulani ya kufunga shughuli ili kupunguza msambao wa virusi vya korona. Kenya, Uganda na Rwanda zilifunga shughuli zote katika vipindi tofauti vya mwaka huku Tanzania ilifunga baadhi ya shughuli lakini ikarejea hali ya kawaida baada ya kipindi kifupi. Serikali za ukanda huu zimefungua uchumi wao polepole lakini kwa umakini ijapokuwa suala hilo linaendelea kuwa lengo kuu kutegemea idadi ya visa vya korona.

Kwa sababu hii, Benki ya Dunia iliripoti kuwa huku nchi za Afrika za Chini ya Sahara zimeweza kudhibiti virusi hivi kwa idadi ya chini ya maambukizo, tandavu linaendelea kuongeza idadi katika maisha na uchumi wa Afrika. Shughuli ya kiuchumi inatabiriwa kuwa itapungua kwa 3.3% mwaka wa 2020, na kuthibitisha kupungua kwa uchumi kwa mara ya kwanza katika miaka 25. Kupungua sana kwa shughuli ya kiuchumi inachangiwa kiasi na matumizi na uwekezaji wa chini katika nchi kwa sababu ya mikakati ya kudhibiti na kupunguza msambao wa virusi vya korona.

Na ni katika utendakazi wa mazingira haya ya uendeshaji ambapo utendakazi wa NMG, hasa katika nusu ya kwanza ya 2020, uliathiriwa sana kwa sababu makampuni na wateja waliamua kuhifadhi pesa wakati wa janga na baadhi ya biashara, ikijumuisha shule na vyuo, zilifungwa.

**Mwaka wa 2020 ambao hautasahaulika, usio kifani na usioweza kulinganishwa. Ulimwengu uliathiriwa na tandavu ambalo kizazi cha sasa hakijawahi kupitia. Tandavu hili limepindua dunia juu chini, na kulazimisha mataifa kadhaa kufunga baadhi ya shughuli au kufunga shughuli zote kabisa.**

## Matokeo ya Kifedha

Shirika lilipata jumla ya mauzo ya shilingi bilioni 6.8 na faida ya kabla ya ushuru ya shilingi bilioni 0.1. (Mwaka wa 2019 ilikuwa ni shilingi bilioni 9.1 na shilingi bilioni 1.3). Mazingira ya uchumi yaliyokandamizwa kutokana na mkurupuko wa tandavu yaliathiri sana utendakazi wa Shirika katika ukanda huu, hasa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka huo.

Sekta nyingine nyingi ziliathiriwa pia kwa njia sawa, na kusababisha watu kupoteza kazi kwa upande mmoja na kupunguza mapato kwa makampuni kwa upande mwingine. Katika nusu ya pili ya mwaka huo Shirika lilisajili kusitawi tena imara katika mikondo yote ya mapato huku televisheni, redio na dijitali zikisajili ukuaji wa tarakimu mbili ikilinganishwa na nusu ya kwanza.

**Tunasherehekea na kukaribisha maendeleo ya kutolewa kwa chanjo za Covid-19 kwa zamu huku pia tukitambua aina mpya za tandavu ambazo zimekuwa hatari kwa juhudi za sasa ili kukabiliana na tishio hili la maisha.**

**Katika nusu ya pili ya mwaka huo Shirika lilisajili kusitawi tena imara katika mikondo yote ya mapato huku televisheni, redio na dijitali zikisajili ukuaji wa tarakimu mbili ikilinganishwa na nusu ya kwanza.**

# Taarifa ya Mwenyekiti (inaendelea)

**2020**
**Shirika lilizindua chapa yake ya kidijitali Nation. Africa inayolenga kuwezesha hadhira katika bara zima kupitia maudhui ya ubora wa juu, kama hatua ya kwanza dhidi ya kuwa kampuni ya kisasa kwa maudhui ya kidijitali, kuchukua uongozi katika mandhari ya uchapishaji wa vifaa vya mkononi katika Afrika na kukuza mapato ya msomaji.**

Utendakazi wa jumla ulifidiwa kiasi na mikakati ya usimamizi wa gharama iliyochukuliwa ili kuboresha ufaafu wa uendeshaji na kuongeza uzalishaji.

## Migao

Shirika limerejelea safari ya mageuzi ya kidijitali inayoanzisha uwekezaji muhimu katika uanahabari wetu na bidhaa zetu za kidijitali. Mnamo mwaka wa 2020 Shirika lilizindua chapa yake ya kidijitali *Nation.Africa* inayolenga kuwezesha hadhira katika bara zima kupitia maudhui ya ubora wa juu, kama hatua ya kwanza dhidi ya kuwa kampuni ya kisasa kwa maudhui ya kidijitali, kuchukua uongozi katika mandhari ya uchapishaji wa vifaa vya mkononi katika Afrika na kukuza mapato ya msomaji.

Awamu inayofuata ya safari ya kidijitali itahitaji rasilimali kadhaa. Hii itajumuisha akiba ya fedha ili kutekeleza mipango. Kwa kuzingatia yaliyo hapo juu, Wakurugenzi hawapendekezi malipo ya mgao wa mwaka uliomalizikia tarehe 31 Desemba, 2020 (2019: Shilingi 1.50 kwa kila hisa).

## Mpango wa Ununuzi wa Hisa

Bodi ya Wakurugenzi wa NMG waliamua kupendekezea washikadau wake kununua hadi asilimia kumi (10%) za mtaji wa hisa yake iliyotolewa na iliyolipiwa katika Mpango wa Ununuzi wa Hisa Zake kwa mujibu wa ushughulikia wa Sheria ya Makampuni na Kanuni za Masoko ya Mtaji (Dhamana) (Ofa za Umma, Uorodheshaji na Ubainishaji), 2002. Hii itawapa washikadau wa NMG chaguo la kuuza uwekezaji wao na kupata pesa. Mpango wa Ununuzi wa Hisa unafuata kanuni na uidhinishaji wa mshikadau.

Ununuzi wa hisa hutokea wakati kampuni inanunua kutoka kwa wawekezaji wake sehemu ya hisa zake zilizotolewa. Ni mojawapo ya njia za kampuni kurudisha fedha kwa washikadau wake, kupunguza kwa ufanisi idadi ya hisa zilizotolewa na kuongeza haki za usawa za hisa yoyote moja. Ununuzi wa hisa hulenga kuwapa washikadau chaguo mbadala wa kuongeza thamani kutoka kwa uwekezaji wao.

## Bei ya Hisa na Utoaji Mtaji kwa Soko

Bei ya hisa ya NMG ilipungua kutoka kwa wastani ya shilingi 39.8 mwishoni mwa mwaka uliotangulia hadi karibu wastani ya shilingi 15.5. Hii ilikuwa kwa sababu ya masoko ya Ubadilishaji wa Dhamana ya Soko la Nairobi (NSE) yaliyotishiwa kila pahali na kuwa na sifa ya mazingira magumu kuendeshea shughuli yaliyosababishwa na tandavu ya Covid-19 na kisha kupungua kwa mapato na kupotea kwa mtaji wa kigeni. Utoaji mtaji kwa soko na Shirika ulikuwa shilingi bilioni kufikia tarehe 31 Desemba, 2020.

## Safari ya Mabadiliko ya Kidijitali

Tandavu hii ilisababisha mabadiliko ya haraka sana na ya mageuzi katika mfumo wa biashara yetu. Hii inajumuisha kuacha mfumo wa urithi wa kutegemea matangazo na mauzo ya nakala za magazeti ili kupata ukuaji wa mapato hadi kwa mapato ya matangazo na msomaji yanayoendeshwa na maudhui yanayowasilishwa kidijitali. Inajumuisha kuchunguza mikondo mingine ya mapato katika matukio na nafasi ya teknolojia.

**Awamu inayofuata ya safari ya kidijitali itahitaji rasilimali kadhaa. Hii itajumuisha akiba ya fedha ili kutekeleza mipango.**

Kwa hali hii, mwaka uliopita ulikuwa ni wenye mabadiliko kwa NMG dhidi ya kuwa kampuni ya kisasa ya maudhui ya kidijitali. Shirika lilipiga hatua ya ujasiri katika safari yake ya mageuzi ya kidijitali kwa uzinduzi wa chapa yake ya kidijitali *Nation.Africa*. Kipengele muhimu ni pamoja na jukwaa lenye ubora wa juu, mwingiliano, linaendeshwa na mtumiaji na lenye vyombo vya habari anuwai; maudhui yenye ubora wa juu, ya kushawishi na anuwai katika bara zima; eneo la soko; matangazo ya habari, video na majarida ya habari.

## Uongozi Kupitia kwa Fikra Mwafaka

### *Majukwaa ya Uongozi wa Nation*

Shirika liliendelea kuendeshwa kupitia kwa muhimu ya majukwaa ya uongozi wake wa fikra katika kuendeleza lengo lake la kuathiri jamii kwa njia chanya. Majukwaa haya yanajumuisha *Nation Leadership Forum (Kenya), Monitor's Thought Leaders Forum (Uganda), na Mwananchi Thought Leadership Forum (Tanzania).*

**Katika kuunga mkono juhudi za jumla za kukabiliana na tandavu hili, Shirika kilikuwa na zaidi ya vikao thelathini (30) vya majukwaa yake katika ukanda huu ili kuchochea muktadha, kuhimiza mazungumzo, kuongoza maoni ya umma, kuathiri sera inayohusiana na Covid-19 na athari zake katika sekta mbalimbali za uchumi.**

Katika kuunga mkono juhudi za jumla za kukabiliana na tandavu hili, Shirika kilikuwa na zaidi ya vikao thelathini (30) vya majukwaa yake katika ukanda huu ili kuchochea muktadha, kuhimiza mazungumzo, kuongoza maoni ya umma, kuathiri sera inayohusiana na Covid-19 na athari zake katika sekta mbalimbali za

# Taarifa ya Mwenyekiti (inaendelea)

uchumi. Hizi zilijumuisha kilimo, uchumi, jinsia, jamii zinazoweza kudhurika, spoti, tasnia ya ubunifu, teknolojia, na vijana.

Tandavu ilileta fursa ya kufanya uvumbuzi huku mikutano ya mtandaoni na mseto kwa haraka ikichukua nafasi ya mkutano wa watu halisi ili kufuata mikakati ya Covid-19 ya kuweka umbali baina yako na watu wengine. Kwa athari yake, majukwaa hayo yalikuwa siyo tu mojawapo ya sauti zinazoaminiwa kuhusu tandavu bali pia vyanzo muhimu vya mapato mbadala kwa Shirika.

> **Shirika limejitolea kuandaa Tamasha la Kusi Linalozingatia Upokeaji wa Mawazo kila mwaka huku likiliimarisha ili liwe jukwaa bora zaidi la mwanzo kabisa barani Afrika litakaloandaliwa katika nchi tofauti Afrika.**

## Tamasha la Kusi Lililozingatia Upokeaji wa Mawazo

Shirika liliendelea kuboresha nafasi yake kama chombo cha kuendesha ajenda ya Afrika kwa *Tamasha lake la Kusi* Lililozingatia Upokeaji wa Mawazo na ambalo, iwapo utakumbuka, lilianzishwa mnamo 2019. Toleo la pili la jukwaa la Afrika Pekee lilitolewa kwa muundo wa mseto, unaojumuisha watu halisi kwa ukumbi na vipengele vya kimtandao kwa walio mbali vilivyokuwa na kauli mbiu ya, "Mpango wa Afrika Baada ya Covid: Kujinufaisha Pamoja". Tamasha hilo lilifanyika Kisumu tarehe 8 na 9 Desemba kwa ushirikiano na Serikali ya Kaunti ya Kisumu. Kongamano hilo lilifanyika katika muda mgumu wakati wa tandavu linaloendelea ili kutathmini athari zake mbaya kwa uchumi na maisha

> **Washiriki 14,000**
> **wajumbe 230 waliweza kuhudhuria ana kwa ana.**

ya Afrika. Lililenga mafanikio yaliyopatikana, lilichunguza ustahimilivu wa Afrika uliodhihirika, na kutabiri jinsi ya kutoka kwa janga hilo.

Tamasha hilo lilivutia wahusika wengi barani Afrika na hata sehemu nyinginezo duniani. Lilihudhuriwa na washiriki 14,000 kwa njia ya mtandao kutoka nchi 44 na majiji makuu 83 na wajumbe 230 waliweza kuhudhuria ana kwa ana. Kimsingi, lilifikia zaidi ya watumiaji milioni 460 wa mtandao wa kijamii katika bara zima. Washirika walikuwa pamoja na mwenyeji-mwenza Rais Uhuru Kenyatta, Rais Paul Kagame (mwenyeji-mwenza 2019), Prof. Anyang Nyong'o, Gavana mweyeji-mwenza, Dkt. Mukhisa Kituyi, aliyekuwa Katibu Mkuu, Kongamano kuhusu Biashara na Maendeleo wa Umoja wa Mataifa, Maimunah Mohd Sharif, Chini ya Katibu Mkuu na Mkurugenzi Mkuu, UN-Habitat miongoni mwa wataalamu kadhaa. Miongoni mwa waliohudhuria pia walikuwa viongozi wa biashara, waundaji sera, wanadiplomasia, wavumbuzi, watafiti, wajasiriamali wadogo, wanafunzi miongoni mwa wengine.

Shirika limejitolea kuandaa *Tamasha la Kusi* Linalozingatia Upokeaji wa Mawazo kila mwaka huku likiliimarisha ili liwe jukwaa bora zaidi la mwanzo kabisa barani Afrika litakaloandaliwa katika nchi tofauti Afrika.

## Ajenda ya Uendelevu

Shirika linaendelea kuhakikisha kwamba uendelevu unabakia kuwa lengo letu kuu, kupitia uhusishaji wa madhumuni ya 'uundaji wa thamani' kama mojawapo ya mihimili muhimu ya mkakati wake wa kibiashara.

Tandavu liliangazia zaidi uhusiano kati ya mazingira na shughuli za binadamu, huku janga la afya likisababisha ukiukaji wa tabia na athari kali kwa biashara. Huku hii ilidhihirika kuleta changamoto kwa biashara kote ulimwenguni, pia iliwezesha dhana ya kuwa biashara haiendeshwi katika mazingira ombwe, mashirika kote ulimwenguni yakija pamoja kuchangia kifedha na njia zisizo za kifedha dhidi ya usimamizi na kuangamizwa kwa tandavu hili.

Kwa sababu hii, Shirika lilishughulikia jukumu muhimu kwenye ukanda mzima na kote barani katika kutoa taarifa na elimu muhimu na kwa wakati unaofaa kwa umma kuhusu tandavu hili. Tunawahakikishia washikadau wetu na Serikali katika Afrika Mashariki kuhusu msaada na ushirikiano wetu katika vita dhidi ya msambao wa Covid-19. Tutaendelea kuwa kwenye mstari wa mbele wa kuripoti kuhusu tandavu na kwa uamilifu ili kuendesha ufahamu katika majukwaa yetu ili kuathiri mabadiliko ya tabia na kuondoa unyanyapaa.

**Shirika linaendelea kuhakikisha kwamba uendelevu unabakia kuwa lengo letu kuu, kupitia uhusishaji wa madhumuni ya 'uundaji wa thamani' kama mojawapo ya mihimili muhimu ya mkakati wake wa kibiashara.**

**Tutaendelea kuwa kwenye mstari wa mbele wa kuripoti kuhusu tandavu na kwa uamilifu ili kuendesha ufahamu katika majukwaa yetu ili kuathiri mabadiliko ya tabia na kuondoa unyanyapaa.**

# Taarifa ya Mwenyekiti (inaendelea)

**Lengo ni kujenga nafasi kamilifu ya uwezeshaji kwenye kazi zote ili kuharakisha mageuzi ya NMG ya kuwa shirika linalotamba kwenye tasnia ya kidijitali ulimwenguni.**

**Tunapoendelea mbele, tunaazimia kujenga biashara mpya kabisa itakayoimarisha ubora kwa kutumia mfumo wa kuanzia chini kwenda juu, maudhui tofauti na yanayohusisha watu na yanayoweza kubidhaishwa kidijitali kwenye vifaa vya mkononi kwa lengo la kuongoza katika mazingira ya uchapishaji wa vifaa vya mkononi.**

### Mabadiliko ya Bodi

Kulikuwa na mabadiliko fulani katika Bodi mwaka jana. Tarehe 15 Februari, Shirika lilimpoteza mmoja wa Wakurugenzi wake, Dkt. Simon Kagugube. Alifariki baada ya kuugua kidogo akiwa na umri wa miaka 65. Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Utawala na Wafanyakazi wa NMG, napendelea kutoa rambirambi zetu kwa familia na wafanyakazi wenzetu. Dkt. Kagugube kwa furaha alihudumu kama mkurugenzi huru wa NMG kuanzia Septemba, 2011. Alikuwa mtaalamu wa mikakati ya ubora, ameacha urithi mkubwa na atakumbukwa kama mfano bora wa kiongozi wa biashara. Alikuwa mfanyakazi wa kiushirika pamoja na rafiki. Tutamkosa sana na mawazo pamoja na maombi yetu yanaendelea kuwa na familia yake.

Bw. Al-Noor Ramji, Afisa Mkuu wa Dijitali wa Prudential PLC katika Shirika, aliteuliwa kujiunga na Bodi mnamo mwezi Machi mwaka jana. Bodi itafaidika pakubwa na tajiriba yake pana katika uongozi wa utekelezaji wa mkakati wa kidijitali kwenye kipindi cha muda mrefu kwa Shirika.

### Watu Wetu

Shirika linaendelea kujitolea katika utambuaji, ukuzaji, na ushughulikiaji wa maarifa mapya yatakayosaidia mkakati wa biashara ili kushinda katika mchakato ya kidijitali. Lengo ni kujenga nafasi kamilifu ya uwezeshaji kwenye kazi zote ili kuharakisha mageuzi ya NMG ya kuwa shirika linalotamba kwenye tasnia ya kidijitali ulimwenguni.

### Mustakabali Wetu

Kuvurugwa kwa biashara kutokana na tandavu kumetufunza mambo muhimu. Kwa kweli, hii ndiyo iliyoharakisha kuwekwa upya kwa biashara na safari yetu ya mageuzi ya kidijitali.

Katika kipindi hiki, kumekuwa na ukuaji mkubwa katika matumizi ya maudhui yetu mtandaoni zaidi ya yale tuliyoyapitia kwenye jukwaa letu la urithi. Hii ni habari njema kwetu kwani inathibitisha kuwa bado kuna haja na dai kubwa sana ya maudhui yenye ubora wa juu.

Hivyo basi, wakati ambapo changamoto yetu kuu imekuwa ni jinsi ya kupata pesa, tumeweka kila juhudi, ikiwa ni pamoja kufanya kazi na wataalamu kutoka kwa vyombo vingine vya habari ambao wamefaulu katika shughuli hii, ili kuboresha na kuharakisha uimarishaji wa uchumi unaoambatana na maudhui yetu ya kidijitali. Idadi ya vyombo vya habari vya urithi vilivyokumbana na changamoto sawa vimefanikiwa kufanya mapito na kujijenga upya kutoka kwa majukwaa ya urithi na kuwa majukwaa mapya ya mfumo wa kushinikiza matumizi ya kidijitali. Tuna ujasiri kuwa tupo kwenye njia sahihi ya kufanya hivyo. Tumeanza kuona hatua zilizochukuliwa awali zikileta matokeo kama vile ukuaji wa haraka wa watumiaji wa mtandaoni waliojisajili na kujiandikisha kwenye *Nation.Africa*.

Tunapoendelea mbele, tunaazimia kujenga biashara mpya kabisa itakayoimarisha ubora kwa kutumia mfumo wa kuanzia chini kwenda juu, maudhui tofauti na yanayohusisha watu na yanayoweza kubidhaishwa kidijitali kwenye vifaa vya mkononi kwa lengo la kuongoza katika mazingira ya uchapishaji wa vifaa vya mkononi. Ubidhaishaji utawezeshwa kwa kubadilisha tabia ya hadhira yetu kutoka kwa utamaduni wa maudhui ya bila malipo na kuwa hadhira ya wanaolipia. Bodi ina imani kuwa hatua zinazochukuliwa zitaleta matokeo mazuri na yanayoweza kuwa endelevu.

Mwaka uliopita ulikuwa wenye changamoto na hatua tulizochukua ili kuendeleza biashara huenda hazingewezekana bila msaada wa kila mara wa wakurugenzi wenzangu kwenye Bodi. Naomba kuwashukuru kwa mchango wao muhimu.

Kwa mwaka kama huo uliokuwa na changamoto tele, pongezi zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wote pamoja wafanyakazi wa NMG kwa kujitolea kwao na jitihada zao za mchwa za kufanya kazi kwa bidii ili kukabiliana vilivyo na nyakati zilizokuwa zenye changamoto nyingi. Hii pia haingewezekana bila msaada na kujitolea kwa dhati kwa washirika wetu wa biashara, wateja na washikadau wengine.

Ahsanteni sana!

**Dkt. Wilfred D. Kiboro**

Mwenyekiti

**Katika kipindi hiki, kumekuwa na ukuaji mkubwa katika matumizi ya maudhui yetu mtandaoni zaidi ya yale tuliyoyapitia kwenye jukwaa letu la urithi.**

nation.africa

nation.africa/News
nation.africa/Counties
nation.africa/Business
nation.africa/Opinion
nation.africa/Sports
nation.africa/Life & Style
nation.africa/Newsletters
nation.africa/Audio
nation.africa/Puzzles

*Media of Africa for Africa*

Nation Media Group
Media of Africa for Africa

www.nationmedia.com